
# YOTE KWA YESU



Pastor James Kalekwa

# YOTE KWA YESU.

*Sehemu ya Dhabihu Binafsi katika kumtumikia Mungu kwenye kanisa la Mahala Pamoja.*

James Kalekwa

## Orodha ya Yaliyomo

Tabaruku ........................................................................ 4

Salamu na Utangulizi ........................................................................ 5

1. Dhabihu ya maombi ........................................................................ 8
2. Dhabihu ya upatikanaji ........................................................................ 10
3. Dhabihu ya Muda ........................................................................ 13
4. Dhabihu ya utii ........................................................................ 15
5. Dhabihu ya utaalamu, ujuzi, maarifa na uzoefu ....... 19
6. Dhabihu ya Mali ........................................................................ 23
7. Dhabihu ya Nguvu ........................................................................ 26
8. Dhabihu ya maisha ........................................................................ 28
9. Dhabihu ya mambo yanayopendeza na kumpa raha mtendakazi ........................................................................ 31
10. Dhabihu ya ufuasi ........................................................................ 34

Kuhusu Mwandishi: ........................................................................ 36

Kuhusu New Vine Church: ........................................................................ 36

Mawasiliano na Mwandishi: ........................................................................ 37

## Tabaruku

Mfululizo wa vitabu hivi vya kieltroniki (e-books) bure kwa kila atakaye; ni himizo la kiungu ndani yangu kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari.

Ninatabaruku kitabu hiki kwa kanisa la Kristo na kwa nchi yangu niipendayo, Tanzania.

Kanisa litashinda na kushamiri zaidi!

Tanzania, ninakupenda kwa moyo wote!

## Salamu na Utangulizi

Mfululizo huu wa vitabu vya kieletroniki ni maono ambayo Mungu ameweka ndani ya mtumishi wake, mume wangu mpenzi, kama namna yake ya kuonyesha shukurani kwa Mungu kwa zawadi ya maisha.

Ninamfahamu mume wangu kama mtu anayempenda Mungu kupitiliza. Yuko tayari kulipia gharama yoyote ile kuonyesha hilo. Ni mtu anayewapenda watu wa Mungu kwa namna ambayo sijawahi kuona. Yamekuwa ni maombi yake kuyagusa maisha ya wengi kwa kadiri inavyowezekana kabla Yesu Kristo hajarudi.

Anapoadhimisha siku ya kuzaliwa kwake **Juni 20**, amekuandikia kitabu hiki, akapangilia na kufanya kipatikane kwako bila malipo yoyote. Nimemwona anavyokesha; wakati mwingine kuamka alfajiri sana au kuchelewa sana kulala ili kukamilisha uandishi. Nimemuona anavyoomba na kuombea wasomaji, anavyojisomea na kutafiti ili kuhakikisha anafanya uwasilishaji wa thamani.

Ningependa tuthamini zawadi hii ambayo sisi wengine tunanufaika nayo bila kulipia gharama:

1. Mshukuru Mungu pamoja nasi kwa zawadi hii ya maisha ya Pastor James Kalekwa kisha muombee maisha marefu na afya njema.
2. Mwandikie ujumbe wa kumsalimu na kumpongeza ukisema ni kwa namna gani huduma

yake imeyagusa maisha yako. Ninajua hili litaufurahisha sana moyo wake.

3. Wafikishie vitabu hivi walau watu hamsini tu. Ni vitabu vinatolewa bila malipo (vimeyagharimu maisha ya mwandishi ili vikufikie).
4. Usiuze vitabu hivi. Tuligundua kuwa kuna watu wanavisambaza kwa malipo ya fedha. Hiyo si sawa. Itakuwa ni kwa hasara yako mwenyewe ukifanya hivyo.

Baada ya kuyasema hayo, nikuhakikishie ya kwamba mtu huyu mkuu wa Mungu amejaa hekima za kiungu na neno ambalo siku zote hutokeza shuhuda maishani mwa wengi. Kwa kusoma kitabu hiki, ushuhuda wako unafuatia. Nikutakie usomaji mwema.

Na heri ya kuzaliwa kwa mpendwa wetu, zawadi ya mbingu kwenye kizazi chetu, Pastor JK.

Frida James Kalekwa (Mama Pastor JK)
Mke wa mwandishi
Juni, 2024
Dodoma, Tanzania

Ufunuo 5:12 *"Wakisema kwa sauti kuu, astahili Mwana-Kondoo aliyechinjwa, kuupokea uweza na utajiri na hekima na nguvu na heshima na utukufu. Na kila kiumbe kilichoko mbinguni na juu ya nchi na chini ya juu ya bahari, na vitu vyote vilivyomo ndani yake, nalivisikia, vikisema, Baraka na heshima na utukufu na uweza una yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na yeye Mwana-Kondoo, hata milele"*

Kuna vitu ambavyo mtu anastahili kupokea aina Fulani ya vitu kwa kuwa wamechinjwa (wamejitoa dhabihu). Kama hakuna kuchinjwa hakuna kustahili.

Kama watendakazi kuna vitu tunavipokea kwa neema, na kuna vitu ambavyo kwenye ufalme huu tunavipokea kwa kulipa gharama kwa kuwa mtoaji (Mungu) alilipia gharamu.

# 1.Dhabihu ya maombi

Dhabihu ni kutenda zaidi ya kawaida, mazoea au zaidi ya ilivyotarajiwa na zaidi ya watu wengine wanavyotenda. Jambo lolote lenye maana hapa duniani linahitaji dhabihu.

Marko 14:35 *"**Akaendelea mbele kidogo**, akaanguka kifudifudi, akiomba ya kuwa, ikiwezekana, saa hiyo imwepuke"*

Dhabihu ya maombi inatoka kwenye kanuni ya kwenda mbele zaidi; ili kuwa kielelezo. Huwezi kuwa kielelezo cha mtu ambaye mko mstari mmoja. Ili uweze kuwaongoza watu au kuwaonyesha kielelezo cha kufuata unapaswa kusogea mbele yao ili wapate mahali pa kutazamia.

Kila mtendakazi anaitwa kuwa mwombezi… mwombezi wa kazi ya Mungu na watu walio ndani ya kazi hiyo. Mwombezi (intercessor) ni mtu ambaye anatenga muda kuomba na kuombea mahitaji ya maombi ya kihuduma au utumishi na mahitaji ya watu wengine.

Wakolosai 4:12-13 *"Epafra. Aliye mtu wa kwenu, mtumwa wa Yesu Kristo, awasalimu, akifanya bidii siku zote kwwa ajili yenu katika maombi yake, ili kwamba msimame wakamilifu na kuthibitika sana katika mapenzi yote ya Mungu. Maana namshuhudia kwamba ana juhudi nyingi kwa ajili yenu, na kwa ajili ya hao walioko Laodokia, na kwa ajili ya hao walioko Hierapoli"*

Dhabihu ya maombi ni pamoja na kufunga zaidi ya ratiba zilizopangwa, na zaidi ya washirika; maombi ya kukesha, maombi ya mnyororo-walinzi, maombi na matendo ya imani. Mtendakazi siku zote yuko mbele ya washirika kwenye eneo hili kwa sababu analisikia joto na anausikia uzito wa kazi mabegani ikilinganishwa na washirika. Kama hayo hayatakusukuma kuomba basi itatupelekea kuanza kuhoji uwezo wako wa kuyaelewa mambo!

Kama huwezi kuomba basi utakuwa huwezi kabisa.

Kama huna muda wa kuomba basi huna muda kabisa.

# 2.Dhabihu ya upatikanaji

Kanisa au taasisi inaweza kuwa na rasilimali zote, lakini bila rasilimali watu hakuna umbali wowote taasisi hiyo itafika. Hakuna mbadala wa watu kwenye taasisi yoyote.

Mwanadamu ndiye huyaendesha mambo mengine yote kwenye taasisi/huduma. Mwanadamu ndiye anayeweza kuongoza miongozo, sera, mikakati, na rasilimali zingine zote.

Mungu anatafuta watu, lakini anatafuta watu wanaopatikana kwanza kabla hata ya watu wanaoweza (God seeks the availables more than the abels first). Mtu anayepatikana hata kama hawezi atamzidi mwenye uwezo ambaye hapatikani. Mungu huwa na kawaida ya kuwajengea uwezo wanaopatikana. Kw kuwa Mungu huitazama mioyo, basi huangalia nia ili kutoa thawabu yake.

Mwitikio wa mtendakazi kwa Bwana ni *"Nipo hapa Bwana"* na sio *"Ninaweza Bwana"* Kimsingi ukiitika

kwa kuonyesha uwezo wako huwa ni ujumbe ni ama haujaelewa ukubwa wa kazi au haujielewi.

Ezekieli 22:30 *“Nami nikitafuta mtu miongoni mwao, atakayelitengeneza boma na kusimama mbele zangu mahali palipobomoka, kwa ajili ya nchi, nisije nikaiharibu, lakini sikuona mtu”*

Mungu anapokwenda kwenye kundi la watu anamtafuta mtu sio watu, kwa sababu uwezo huwa ni mwingi kuliko upatikanaji.

Watu ambao huwa wanapatikana Mungu huwa anawaongezea uwezo. Mtu asiyekuwepo na mtu asiyepatikana wanafanana, na mfanano wao ni kuwa hawawezi kutumainiwa. Usipopatikana ni sawasawa na haupo.

Hebu linganisha huyu ndugu mtendakazi kwenye nyakati mbili tofauti alizoitikia jukumu alilopoewa kufanya.

*“Basi akatazama huko na huko, na alipoona ya kuwa hapana mtu, akampiga Mmisri yule, akamficha ndani ya mchanga.”* Kutoka 2:12

*"Musa akamwambia Mungu, Mimi ni nani, hata niende kwa Farao, nikawatoe wana wa Israeli watoke Misri?"* Kutoka 3:11

Kupatikana ni

- Kuwepo kwenye eneo la Kijiografia – eneo la tukio.
- Kuwepo kwenye muda
- Kuwepo kwenye roho – kushiriki ile hali ya hewa. Kuwa na hisia, moyo, namna

Kwa kutambua ya kwamba maombi huwa hayajiombi.

Mahubiri huwa hayajihubiri.

Nyimbo huwa hazijiimbi.

Vifaa vya usafi huwa havifanyi usafi vyenyewe.

Hii inalazimu upatikanaji wa watendakazi wanadamu kwa ajili ya kuzima maana ratiba, vifaa, taratibu na kila kitu.

# 3.Dhabihu ya Muda

Wataalamu wa sayansi ya muda wanaamini kuwa ukitaka kupima utakua nani, unapima huwa unatumia nini na muda wako. Wapi unaelekeza muda wako kuna amua utakua nani. Kutokea kwenye uelewa huo, basi kigezo cha muda kwenye utendakazi ni cha kuzingatiwa sana. Huwezi kuwa unajibu "Tupo pamoja!" halafu hutoi muda kwa ajili ya kazi ya Bwana.

Mungu anatutaka kuwekeza muda mwingi kwenye kazi yake kama tunataka kuona ustawi wa kanisa la mahala pamoja na ufalme wa Mungu duniani.

Matendo 20:31 *"Kwa hiyo* ***kesheni****, mkikumbuka ya kwamba* ***miaka mitatu, usiku na mchana****, sikuacha kumwonya kila mtu kwa machozi"*

Luka 2:37 *"Naye ni mjane wa miaka themanini minne; haondoki katika hekalu,* ***ila huabudu usiku na mchana*** *kwa kufunga na kuomba"*

Mungu huwa anatoa thawabu kwa tabia; Mungu unazingatia na kutaka ubora zaidi kuliko wingi, na kama anataka wingi anataka wingi bora.

Si kwamba Mungu ni muhitaji wa tukio moja kubwa ambalo litafuatiwa na hali ya ukawaida. Si afya sana kufanya mkesha mmoja mkubwa mara moja usiofuatiwa au usiotokana na mikesha mingine.

Mahali unapowekeza muda wako kama mtendakazi panaonyesha mahali unapopathamini.

Muda unakuwa dhabihu kwa sababu masaa huwa ni yaleyale ishirini na nne na yanahitajiwa na watu wako wa karibu, kazi, muda wako binafsi wa kupumzika. Ukiutoa huo muda, hiyo ni dhabihu!

Huwezi kuwa mtendakazi wa thamani kwa utoaji wa kiwango kilekile cha muda kwa kiwango cha washirika au watu tnaowahudumia.

# 4.Dhabihu ya utii

Bwana wetu Yesu Kristo ametuachia kielelezo kikubwa sana cha utii. Kuanzia kwenye nia mpaka kwenye tendo. Utii, kwa muktadha huu, ni kusalimu (submit) matakwa, nia, utashi, vionjo, na ratiba zako kwenye mamlaka unayoifuata ili kuendea kusudi kubwa na linalostahili kufuatwa (worthwhile goal).

*“Mwenyewe akajitenga nao kama kiasi cha kutupa jiwe, akapiga magoti akaomba, akisema, Ee Baba, ikiwa ni mapenzi yako, uniondolee kikombe hiki;* ***walakini si mapenzi yangu, bali yako yatendeke****.”* Luka 22:41-42

Unaona namna Bwana Yesu anayapima maombi, matamanio na matakwa yake kwa lengo kubwa la BABA? Huo ndiyo utii.

Pia, utagundua ni utii katika ngazi ya uneni. Inawezekana ana maoni au muono wake. Lakini kwa sababu ya lengo linalostahili kufuatwa, Bwana Yesu anatuonyesha kielelezo hapa:

*"Kwa sababu mimi sikunena kwa nafsi yangu tu; bali Baba aliyenipeleka, yeye mwenyewe ameniagiza nitakayonena na nitakayosema"* Yohana 12:49

Halafu kwenye ngazi ya tendo, Bwana Yesu anatuonyesha ni kwa namna gani alitenda kwa uendelevu sawasawa na kusudi la Baba. Tunajua kufa msalabani si kama kula kipane cha keki… siyo sherehe. Lakini alikaa hapo.

Wafilipi 2:8 *"tena, alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba"*

Biblia inasema alijinyenyekeza sio alinyenyekezwa! Kwa hiyo, inatupa kuona utii siyo jambo analofanya mtu kama asiye na akili au mtu mjinga na asiyewaza vizuri. Bali hutokea kwa mtu mwenye ufahamu ambaye angeweza kuchagua vinginevyo na bado angekuwa sawa tu. Ndiyo maana huwa ninasema ufuasi… utii… unyenyekevu ni tendo la watu wenye nguvu na uwezo mkubwa sana. Watu duni na dhaifu hawawezi. Ukiona unahangaika kutii ni ujumbe ya kwamba wewe ni duni na dhaifu kwa ndani.

"Vivyo hivyo ninyi vijana, watiini wazee. Naam, ninyi nyote ***jifungeni unyenyekevu***, mpate kuhudumiana; kwa sababu Mungu huwapinga wenye kiburi, ***lakini huwapa wanyenyekevu neema***. ***Basi nyenyekeeni*** chini ya mkono wa Mungu ulio hodari, ili awakweze kwa wakati wake;" 1 Pet 5:5-6

Hakuna wa kukunyekeza mpendwa. Fanya mwenyewe. Kama huwezi, basi huwei kuwa mtendakazi.

Utii huu unapaswa kwanza kumwelekea Mungu, Kulielekea Neno la Mungu, na utii kuelekea uongozi wa kanisa kwa ujumla na maono yanayowaongoza, na uongozi wa kanisa la mahala na taratibu zilizowekwa. Unafanya hayo hali ukijua ya kwamba namna ambavyo Mungu huwachunga watu ni kwa njia ya watu!

Tunachokiitikia katika utii ni mamlaka sio umbo, elimu au umri.

Mimi binafsi nimekuwa mwamini mkubwa wa siri na dhabihu hii. Nimeona namna imekuwa baraka kwa mwili wa Kristo, kanisa na maono, kanisa la mahala na nimeona thawabu kupita maelezo.

Aina za utii ambao sio mzuri

a) Uliocheleweshwa – Pale mtendakazi anapojichagulia muda wa kutii. Ndiyo anatii lakini baada ya muda kupita. Ni utii usio na faida. Utendakazi umefungamanishwa na muda.
b) Pungufu – Huu ni utii lakini kwa kuchagua na kubagua. Hapa mtendakazi anachagua nini cha kutii na nini si cha kutii. Ni kama yuko kwenye *"buffet"*
c) Uliolazimishwa – Hata mtendakazi anatii kwa kuwa hana namna sasa. Lakini kama angekuwa na chaguo jingine angeliendea. Usiwahi kusahau hii shule, utii ni tendo la hiyari.
d) Utii wa sirini lakini si hadharani – Kuwa mtendakazi ni swala la hadhara. Huwezi kuwa mtii kwa kusema unatii hadharani lakini unaona haya au huna ujasiri kusema hadharani.

# 5.Dhabihu ya utaalamu, ujuzi, maarifa na uzoefu

Mungu anataka baada ya kupatikana tutote utaalamu, ujuzi na uzoefu kwa ajili ya kumtumia kwenye kanisa la mahala pamoja. Mungu hatumikiwi na ubongo butu. Utumishi siyo sehemu ya watu wajinga.

*"BWANA akanena na Musa, na kumwambia, 2Angalia, nimemwita kwa jina lake Bezaleli mwana wa Uri, mwana wa Huri, wa kabila ya Yuda; 3nami nimemjaza roho ya Mungu, katika hekima, na maarifa, na ujuzi, na mambo ya kazi ya kila aina, 4ili abuni kazi za ustadi, kuwa fundi wa dhahabu, na wa fedha, na wa shaba, 5na kukata vito kwa kutiwa mahali, na kuchora miti, na kufanya kazi ya ustadi iwayo yote. 6Tena, tazama, nimemchagua, awe pamoja naye, huyo Oholiabu, mwana wa Ahisamaki, wa kabila ya Dani; nami nimetia hekima katika mioyo ya wote wenye moyo wa hekima, ili wapate kufanya vyote nilivyokuagiza."* Kutoka 31:1-7

Mungu alipotaka kujengewa hema yakukutania alimuita fundi mkuu aitwaye Bezaleli mwana wa Uri akisaidiwa na Oholiabu mwana wa Ahisamaki. Hawa walileta ujuzi na maarifa kwenye ukiroho ili kuzaa ubora.

*"Kwa* ***hekima BWANA aliiweka misingi ya nchi;*** *Kwa akili zake akazifanya mbingu imara;"* Mithali 3:19

Mungu huhusisha hekima katika utendaji wa kazi zake. Usidhani ukiroho ni kufanya vitu bila kutumia ujuzi, ubunifu, maarifa au uhusisha namna yoyote ile ya kiakili.

Ni kweli daraja la kwanza la lazima la kuingilia kwenye utendakazi ni upatikanaji (availability) hata hivyo baada ya Mungu kukuthibitisha atahitaji utumie uweo (ability) katika kumtumikia. Lazima kuwe na uwiano wenye afya baina ya hayo.

Ukifuatilia huduma na utumishi wa mtume Paulo ulikuwa umezungukwa na kupambwa na watendakazi wenye ujuzi na walio tayari kutoa dhabihu yao ya ujuzi kusababisha ufalme wa Mungu uende mbele. Si ajabu matokeo ya mtume yalikuwa makubwa kiasi kile.

Tito 3:13 *"Zena,* ***yule mwanasheria****, na Apolo, uwasafirishe kwa bidi, wasipungukiwe na cho chote"*

2Timotheo 4:14 *"Iskanda,* ***mfua shaba*** *alionyesha ubaya mwingi kwangu; Bwana atamlipa sawasawa na matendo yake"*

Matendo 16:14 *"Mwanamke mmoja,* ***jina lake Lidia, mwenye kuuza rangi ya zambarau****, mwenyeji wa Thiatira, Mcha Mungu …"*

Wakolosai 4:14 *"Luka,* ***yule tabibu mpendwa****, na Dema wanawasalimia"* (Luka 1:1, Mdo 1:1)

Hiyo ni mifano kutoka kwenye huduma ya kitume ya Paulo lakini Biblia imejaa mifano ya namna hii pahala pengi.

Kwa nini ujuzi na ufahamu ni dhabihu? Ni kwa sababu, kuna muda mbao umeajiriwa au umejiajiri mwenyewe ambapo ujuzi huo unatumika. Inawezekana gharama za kuulipa ujuzi huo ni kiasi fulani cha fedha. Inawezekana baada ya kuutumia ujuzi huo kwenye eneo husika ungependa kurudi nyumbani na kupumzika au kubadilisha aina ya kazi.

Sasa, kazi ya Mungu inafika mahali inahitaji matumizi ya ujuzi wako kama sadaka yako kwa Bwana Yesu. Hiyo ni dhabihu!

Kama mtendakazi, unapaswa kujua hiyo ni mila na desturi na si swala la kujadiliana. Huwezi kuwa mtendakazi ambaye hautoi dhabihu ya ujuzi. Kwa hiyo, angalia ni kwa jinsi gani utaalamu wako unaweza kuliboresha kanisa la mahala pamoja, idara fulani ndani ya kanisa au namna ya kutenda mambo ya siku kwa siku ya kanisa.

Tazama ni kwa jinsi gani unaweza kumshauri mchungaji… kushauri viongozi wako wa idara… au kufanya jambo kwa vitendo ili kuweka kielelezo. Yale matokeo unayoyazalisha kule ofisini au eneo lako la kazi, basi yazalishe hapa kwenye nyumba ya Bwana.

# 6.Dhabihu ya Mali

Kazi yoyote ya maana kwa hao wanaoifanya inataka uwekezaji wa mali sana, kazi ya Mungu ni kazi ya maana kuliko zote na inahitaji mali.

Uhitajikaji wa mali kwenye kazi ya Mungu sio kwamba tunamsaidia au kumfadhili Mungu bali ni namna ya Mungu kutushirikisha baraka zitokanazo na kazi yake.

Kutoka 10:9 *"Musa akamjibu, tutakwenda na vijana wetu, na wazee wetu, na wana wetu, na binti zetu,* ***tutakwenda na kondoo zetu na ng'ombe zetu****; kwa kuwa inatupasa kumfanyia BWANA sikukuu"*

Bwana ametuita kama watendakazi wazimawazima na kila kitu tulichonacho. Kumbuk kanuni ya kiroho ni kuwa mahali hazina yako ilipo ndipo na moyo wako ulipo. Mali zilipo mtu atakwenda.

Mtendaji asiyetoa ni mtendaji asiyekuwepo; kama huwezi kutoa kwenye hayo maono huwezi kuwepo kwenye hayo maono; utendakazi kwa njia ya mali unaonyesha hali ya moyo wa mtu. Uelekeo wa moyo wa mtu. Ni kipimo

kwako mwenyewe kama mtendakazi kujiambia umo au la!

Nimekuwa nikiwafundisha hapa kila mara ya kwamba hakuna mtu asiye na kitu kabisa kiasi chakukosa cha kutoa. Na hakuna mtu mwenye vitu vyote kiasi cha kutoa kutimiliza hitaji lote la huduma. Kila mtu… kila mtendakazi anapaswa kutoa mali kwa kazi ya Bwana.

Kutoka 10:25-26 *"Musa akasema, Ni lazima utupe mikononi mwetu na wanyama wa dhabihu, na wa sadaka za kuteketezwa, ili tupate kumchinjia BWANA Mungu wetu dhabihu. Makundi yetu pia watakwenda pamoja nasi; hautasalia nyuma hata ukwato mmoja**; kwa maana inampasa kutwaa katika hao tupate kumtumikia BWANA, Mungu wetu; nasi hatujui, hata tutakapofika huko, ni kiotu gani ambacho kwa hicho inatupasas kumtumikia BWANA**"*

Tunamtumikia Mungu na chochote anachotaka tukitumie nacho kumtumikia. Mungu anachokitaka ndicho kinapaswa kutolewa. Kila mtendakazi ana kitu cha kutoa, hakuna mtendakazi asiyekuwa na kitu cha kutoa kwa

sababu hakuna utoaji au kitu kidogo kisichostahili kutolewa kwa Mungu.

Angalia uelewa wa Musa Musa kuhusu kumtolea Bwana. Anasema hatujui ni kitu gani Bwana anaweza kukitaka ili kwacho tumtumikie.

Akitaka fedha… akitaka nyumba… akitaka kiwanja… akitaka gari… akitaka TV Screen… akitaka simu. Mungu anatumikiwa kwa mali zetu.

Mtririko huu wa utumishi utauona kwenye huduma ya Bwana Yesu na utendaji wake alipokuwa hapa duniani. Kuna watendakazi pamoja naye ambao wao walitambua alichokibeba wakaamua kusimama nacho kwa mali.

Mathayo 27:55 *"Palikuwa na wanawake wengi pale wakitazama kwa mbali, hao ndio waliomfuata Yesu toka Galilaya na kumtumikia"*

Luka 8:3 *"na Yoana mkewe Kuza, wakili wake Herode, na Susana, na wengine wengi waliokuwa wakimhudumia kwa mali zao"*

# 7.Dhabihu ya Nguvu

Dhabihu ya nguvu ni msuli wa mwili, bidii (diligency) ya mtendakazi kufanya kwa kumaanisha, kulazimisha matokeo. Hii inajumuisha matumizi ya nguvu za mwili kwenye nyumba ya Mungu na utumishi kwa ujumla. Kuna nyakati ambazo Mungu anakutarajia uachilie dhabihu ya namna hii.

Unakumbuka wakati wa Nehemia na ujenzi wa ukuta wa Yersulameu? Wayahudi ndiyo walikuwa watendakazi kwenye shughuli za kutumia nguvu.

Yeremia 48:10 *"Na alaaniwe* ***mtu afanyaye kazi ya BWANA kwa ulegevu****; na alaaniwe auzuiaye upanga wake usimwage damu"*

Mhubiri 10:18 *"Kwa sababu ya uvivu paa hunepa; na kwa utepetevu wa mikono nyumba huvuja"*

Kazi ya Mungu inagharimu damu ya Yesu. Pia kazi ya huduma itagharimu jasho, nguvu, bidii ya watendakazi.

*“Kesheni, simameni imara katika Imani,* ***fanyeni kiume, mkawe hodari.****”* 1 Kor 16:13

Hii inaonyesha kiwango cha nguvu kinachotakiwa kuwekezwa kwenye utendaji. Kuna namna hili neno “fanyeni kiume” linapendekeza kwamba kuna uhusikawa nguvu.

Unakumbuka Bwana Yesu alichokisema kuhusu alipokuwa akijibu kuhusu amri iliyo kuu katika Torati?

*“Akajibu akasema, Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote,* ***na kwa nguvu zako zote,*** *na kwa akili zako zote; na jirani yako kama nafsi yako.”* Luka 10:27

Kile kinachoendelea moyoni mwako kumuhusu Mungu basi ruhusu kionekane mwilini mwako kwa njia ya nguvu.

# 8.Dhabihu ya maisha

Utendaji wa huduma kuna nyakati unakuwa na shughuli nyingi na zinazotinga sana kiasi kama cha kusikia uhai wako unatoka. Kuna nyakati ambazo kuwa mtendakazi kunachukua muda wako wa mapumziko, muda wako wa kujichanganya na wenzako kazini au kwenye jamii… hiyo ni dhabihu.

Vilevile, utendaji wa huduma huvia vita, mashambulio na matisho. Vinaweza kuwa vinaelekezwa kwenye kazi ya Mungu au vingine vinaelekezwa kwa mtumishi ambaye anawaongoza. Kazi na jukumu la mtendakazi ni kuilinda kazi ya Mungu na mtumishi wa Mungu.

Haujafika kiwango hiki, bado hauwezi kuwa mtedakazi kiasi cha kuzalisha matokeo anayoyatarjia Mungu kwenye kazi yake.

Unajua iongozi wa kanisa la mahali pamoja ni taa ya kanisa la mahali pamoja. Kama mtendakazi anapaswa kuilinda taa ya kanisa isizimike kwa gharama ya uhai.

Kuna vita ambazo kama mtendakazi anapaswa kuzipigana kulinda kanisa la Mungu na kulinda mchungaji –taa. Vita za maneno/uzushi na kuna vita ambazo zitataka kugharimu uhai

Warumi 16:3-4 *"Nisalimieni Priska na Akila, watenda kazi pamoja nami katika Kristo Yesu;* ***waliokuwa tayari hata kukatwa kichwa kwa ajili ya maisha yangu****; ambao ninawashukuru, wala si mimi tu, ila na makanisa ya mataifa yote pia; nisalimieni na kanisa lililomo katika nyumba yao"*

Dhabihu ya uhai ni kuwa tayari kukinga kifua chao kwa ajili ya maisha ya mtumishi wa Mungu.

Mathayo 26:35 *"Petro akamwambia,* ***ijaponipasa kufa nawe, sitakukana kamwe****. Na wanafunzi wote wakasema hivyo hivyo"*

Ufunuo 2:10 *"Usiogope mambo yatakayokupata tazama, huyo ibilisi* ***atawatupa baadhi yenu gerezani ili mjaribiwe, nanyi mtakuwa na dhiki siku kumi.*** *Uwe* ***mwaminifu hata kufa****, nami nitakupa taji ya uzima"*

Kama watu walitoa damu kwa ajili ya injili hakuna kitu ambacho huwezi kukitoa kwa ajili ya Injili.

Kiwango cha uaminifu kinachotafutwa kwenye kitabu cha Ufunuo ni kiwango cha *"hata kufa…"* ambayo tafsiri yake ni kwamba kama itagharimu uhai wako basi baki kuwa mwaminifu kwa Mungu na kwa kazi yake.

*"Naye Ishi-benobu, aliyekuwa mmojawapo wa Warefai, ambaye uzito wa mkuki wake ulikuwa shekeli mia tatu za shaba kwa uzani, **naye amejifungia upanga mpya, alijaribu kumwua Daudi**. Lakini Abishai, mwana wa Seruya, akamsaidia, akampiga Mfilisti, akamwua. **Ndipo watu wa Daudi wakamwapia, wakasema, Wewe hutatoka tena pamoja nasi kwenda vitani, usije ukaizima taa ya Israeli.**"* 2 Samweli 21:16-17

Hili ni neno zito sana… watendakazi walimtazama kiongozi wao kama taa. Waliingia kumlinda katikati ya pigano kisha kujiapiza ya kwamba kuna vitu hatafanya bali wao watafanya ili kuilinda taa ya Israeli.

# 9.Dhabihu ya mambo yanayopendeza na kumpa raha mtendakazi

Ufunuo 5:12 *"Wakisema kwa sauti kuu, astahili Mwana-Kondoo* ***aliyechinjwa****, kuupokea uweza na utajiri na hekima na nguvu na heshima na utukufu. Na kila kiumbe kilichoko mbinguni na juu ya nchi na chini ya juu ya bahari, na vitu vyote vilivyomo ndani yake, nalivisikia, vikisema, Baraka na heshima na utukufu na uweza una yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, nay eye Mwana-Kondoo, hata milele"*

Usisahau dhabihu ni kusalimu matakwa yako kwa ajili ya kutimiza unayotakiwa kuyatimiza; kwenye utumishi lazima kutoa vitu ambavyo tunavipenda… vinatufurahishwa… vinatupa raha na burudiko. Bwana Yesu mwenyewe angependa uhai wake. Angependa kuendelea kuwepo na wanafunzi wake. Lakini aliisalinu roho yake!

Luka 9:49-61 *“Akamwambia mwingine, Nifuate. Akasema, Bwana, nipe ruhusa kwanza niende nikamzike baba yangu. Akamwambia waache wafu wawazike wafu wao; bali wewe enenda ukautangaze ufalme wa Mungu. Mtu mwingine pia akamwambia, Bwana, nitakufuata; lakini nipe, ruhusa kwanza nikawaage watu wa nyumbani”*

Kuna kitabu nimeandika kuhusu “Acha Wafu Wawazike Wafu Wao.” Kinafafanua dhana ya jambo alilolizungumzia Bwana Yesu. Hebu ngoja nikuonyeshe mifano mingine hapa ili uone ambavyo utendakazi unataka uuendee kwa gharama ya yale unayoyapenda.

*“akamtuma mtumwa wake saa ya chakula awaambie wale walioalikwa, Njoni, kwa kuwa vitu vyote vimekwisha kuwekwa tayari. 18Wakaanza wote kutoa udhuru kwa nia moja.* ***Wa kwanza alimwambia, Nimenunua shamba, sharti niende nikalitazame;*** *tafadhali unisamehe. 19Mwingine akasema,* ***Nimenunua ng’ombe jozi tano, ninakwenda kuwajaribu;*** *tafadhali unisamehe. 20Mwingine akasema,* **Nimeoa mke, na kwa sababu hiyo siwezi kuja.** *21Yule mtumwa akaenda, akampa bwana*

*wake habari ya mambo hayo. Basi, yule mwenye nyumba akakasirika, akamwambia mtumwa wake, Toka upesi, uende katika njia kuu na vichochoro vya mji, ukawalete hapa maskini, na vilema, na vipofu, na viwete."* Luka 14:17-21

Huu ni mfano kuhusu ufalme wa Mungu ukisoma kuanzia mistari inayotangulia. Halafu tazama mwitikio wa yule aliyendaa sherehe. Hakusema, "Ooh ninaelewa. Ni maswala ya kibinadamu tu!" Alikasirika!

Nikuambie mpendwa, ukiwamtendakazi kwenye ufalme, "Tafadhali unisamehe!" siyo msamiati wa kistaarabu. Kwenye ufalme huu visingizio havikubaliki na havivumiliki. Mtendakazi mwenye visingizio vingi huwa anaachwa na wanageukiwa wengine ambao kimsingi hawakuwa hata wamewaziwa au kustahili kwa namna yoyote ile.

Kumbuka hili maelezo mengi hayakamilishi kazi! *"You know, you know"* zikiwa nyingi, huufai utumishi huu. Unaweza kuendelea kupokea na kuhudumia siyo kuwa mtendakazi.

# 10. Dhabihu ya ufuasi

Kila mwanadamu ana mbegu ya uongozi ndani yake ambao humsukuma kujiongoza yeye mwenyewe. Hata hivyo baada ya anguko, hali ya ubinafsi imeingia na kujiwasilisha kama ile mbegu ya uongozi. Hii imefanya swala la ufuasi kuwa gumu kwa kuwa na aina hiyo ya mchanganyiko ndani yake. Na baada ya dhambi hali hii imeongezeka na kupelekea kila mtu kutaka kujitawala na kujiongoza mwenyewe. Hitimisho langu ni kwamba mwanadamu anayeweza kufuata, ni mwanadamu aliyejidhabihu.

Nimeandika vitabu vyenye mada hii: **"Kuwa Mfuasi wa Mtu"** na **"Mfuasi Mfano wa Epafradito"** vinaweza kukusaidia kuielewa kwa kina dhana hii ya ufuasi.

Nitaweka ripoti ya kiongozi kumuhusu mfuasi wake ndipo usaidike kuona umbali na kina cha ufuasi unavyopaswa kuwa:

*"Bali **wewe umeyafuata** mafundisho yangu, na mwenendo wangu, na makusudi yangu, na imani, na*

*uvumilivu, 11na upendo, na saburi; tena na adha zangu na mateso, mambo yaliyonipata katika Antiokia, katika Ikonio, na katika Listra, kila namna ya adha niliyoistahimili, naye Bwana aliniokoa katika hayo yote."* 2 Timotheo 3:10-11

Unaona kuna idadi ya mambo aliyoyafuata:

i. Mafundisho
ii. Mwenendo
iii. Makusudi
iv. Imani
v. Uvumilivu
vi. Upendo
vii. Saburi
viii. Adha
ix. Mateso

Wengi hufuata mambo yanayovutia na kusherehesha tu. Ongeza kwenye orodha yako kama mtendakazi. Unahesabika na kiongozi wako kuwa ni mfuasi ikiwa utaenda umbali huu. Pungufu ya hao, haipokelewi.

**Kuhusu Mwandishi:**
Mwandishi wa kitabu hiki, James Kalekwa, ni mfuasi wa Yesu Kristo; mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; Mume mpenzi wa Frida, baba anayewajibika wa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla; na anafurahia kuwa mchungaji mkazi wa kanisa la New Vine jijini Dodoma.

Mchungaji James ameitwa *"Kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari."* [Habakuki 2:14]

**Kuhusu New Vine Church:**
Kanisa la New Vine limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitakacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa. (Mathayo 5:13-14/Yoeli 2:2-11)

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz

**Mawasiliano na Mwandishi:**



# NEW VINE CHURCH | Dodoma



New Vine Church limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa *(Mathayo 5:13 -14/Yoeli 2:2 - 11).*

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz



**Mahali tulipo:** Swaswa mkabala na geti la Waziri Mkuu, Dodoma mjini.

**Ratiba za Ibada**

**Alhamisi** Saa 11:15 jioni - saa 12:15 jioni

**Jumapili** Saa 3:00 asubuhi - saa 6:30 mchana

nvc_dodoma   +255 754 917 764

# KUHUSU MWANDISHI



James Kalekwa ni amemwamini Yesu kuwa BWANA na Mwokozi wa maisha yake. Ni mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; ni mume mpenzi wa Frida; baba anayewajibika kwa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla. Ni mchungaji wa New Vine Church - Dodoma


pastorjameskalekwa

+255 754 917 764

pastorjameskalekwa

pastorjameskalekwa

pastorjameskalekwa

pastorjameskalekwa

MchungajiJK

+255 754 917 764